HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA
MHE. CHARLES N. KEENJA (MB.) WAKATI WA
UZINDUZI WA MKUTANO WA WAKULIMA WADOGO WA CHAI,
TAREHE 25 MACHI, 2003

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunikaribisha kufungua mkutano wenu. Mkutano huu ni fursa nyingine muhimu ya kukutana ili kujadili na kutathmini maendeleo ya zao la chai nchini na mchango wa wakulima wadogo katika maendeleo ya zao hilo.

2. Zao la Chai ni moja kati ya mazao muhimu sana katika lile kundi la mazao tunayoyaita ya **biashara** (mazao yanayozalishwa kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi). Zao la Chai huliingizia Taifa wastani wa USD. 28 milioni kwa mwaka (sawa na Tshs. 22 bilioni).

3. **Mhe. Mwenyekiti,** kwa miaka mingi sasa uzalishaji wa chai umekua haukui na umegota kwenye wastani wa tani 25,000 tu kwa mwaka, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 10 tu ya uzalishaji wa Kenya. Zipo sababu nyingi zilizosababisha hali hii lakini sababu hizo hazibadilishi ukweli kwamba ukuaji wa uzalishaji wa chai nchini umedumaa.

4. Uzalishaji wa Chai ulidumazwa na usimamizi mbovu, uwekezaji mdogo na kutokuwapo kwa mipango madhubuti ya kuendeleza zao hilo. Mwaka jana, Bodi ya Chai Tanzania, ikishirikiana na wadau wa chai, iliandaa mkakati wa kuendeleza zao la chai nchini. Nimeambiwa kwamba mtaujadili mkakati huo katika kikao hiki na nawaomba muujadili kwa makini na kuanza kufikiria mipango ya kuutekeleza.

5. Miongoni mwa mambo muhimu ya kujadiliwa na kuwekewa utaratibu wa utekelezaji ni pamoja na utaratibu wa kuongeza uzalishaji wa wakulima wadogo kwa hekta kutoka uzalishaji wa sasa wa wastani wa kilo 470 kuelekea uzalishaji wa kilo 5,500 unaofnaywa kwenye mashamba makubwa. Ili kuwawezesha wakulima wadogo kuongeza uzalishaji, itabidi kuwahakikishia masoko yenye bei nzuri, kuweka utaratibu utakaowahakikishia upatikanaji wa pembejeo, kuwapatia huduma nzuri za ugani na mafunzo ya kilimo bora cha chai na kuwawekea miundombinu mizuri ya mawasiliano, hususan barabara na simu.

6. Serikali inaandaa utaratibu wa kugharamia kilimo, ambao miongoni mwa mambo mengine, utaweka utaratibu wa kuwapatia wakulima mikopo ya kilimo. Kwa upande wa zao la chai, uzoefu tuliopata katika mashamba ya Mwakaleli na Katumba ya Tukuyu unaonyesha kwamba wakulima wakubwa na/au viwanda vya chai vinaweza kuwasaidia wakulima wadogo kwa kuwapatia masoko ya uhakika kwa chai yao, kuwakopesha pembejeo za kilimo na hata kuwapa ushauri juu ya kilimo bora cha chai. Ningependa kuchukua nafasi hii kuyashukuru makampuni yote ambayo

yameweka utaratibu wa kuwasaidia wakulima wadogo wanaowazunguka na kuhimiza wale ambao hawajaanza kufanya hivyo, kuweka utaratibu kama huo.

7. **Mhe. Mwenyekiti,** pamoja na kusubiri utaratibu wa kugharamia kilimo unaoandaliwa na Serikali na kuwashawishi wenye mashamba makubwa na viwanda vya kusindika chai kuwapatia wakulima wadogo mikopo ya kilimo cha chai, ni muhimu sana kwa wakulima wadogo **kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa.** (SACCOS). Pamoja na kukusanya michango ya wanachama na malipo ya mikopo, Vyama vya kuweka na kukopa vitaweza kukopa kutoka kwenye vyombo vya fedha kwa gharama nafuu na kukopesha wanachama wao. Vyama vya Kuweka na Kukopa vimeanza kuonyesha mafanikio makubwa katika maeneo mengi vilikoanzishwa. Jukumu la Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai ni kuhimiza kuanzishwa kwa Vyama vya Kuweka na Kukopa lakini muhimu zaidi ni kuhakikisha kwamba vinaendeshwa kitaalam na kwa uaminifu wa hali ya juu sana.

8. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** ubinafsishaji umefanikiwa sana katika sekta ya chai. Wanunuzi wa baadhi ya mashamba na viwanda wamevikarabati na kuongeza sana ufanisi wa uzalishaji. Baadhi ya mashamba ambayo yalikuwa yamekufa sasa yamerudia tena uzalishaji na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Tanga zimerudia tena umaarufu wa kuwa wazalishaji muhimu wa chai. Nawapongeza wote walionunua mashamba na viwanda vya chai ambao wanaviendesha kwa ufanisi mkubwa kuliko ilivyokuwa kabla ya ubinafsishaji.

9. Wakati huo huo, wapo watu walionunua mashamba na viwanda vya chai ambao wanaviendesha vibaya sana. Mashamba ya aina hii ni pamoja na Maruku, lililoko mkoani Kagera, Dabaga lililoko Iringa na Lupembe lililoko Njombe ambalo linakabiliwa na migogoro ya ubinafsishaji isiyokwisha.

10. Serikali inatathmini upya ubinafsishaji wa mashamba na viwanda hivi na iwapo hali iliyopo haitabadilika katika miezi mitatu ijayo, mikataba ya mauzo itasitishwa na hatua kuchukuliwa zitakazowezesha mashamba hayo kubinafsishwa kwa watu wenye uwezo na ujuzi wa kuyaendesha kwa ufanisi. Aidha, kama walioomba kununua mashamba na viwanda hivyo wanaona kwamba hawamudu kuviendesha, ni busara kwao kuvirudisha serikalini ili vibinafsishwe upya, vinginevyo, itabidi wasaidiwe kufikia uamuzi huo. Hizi ni mali za umma wa Tanzania na ni lazima ziendeshwe kwa manufaa ya umma.

11. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Tanzania ina maeneo mengi na makubwa yanayofaa kwa upanuzi wa kilimo cha chai. Maeneo ya aina hiyo yako kwenye mikoa ya Iringa na Mbeya ambako tayari chai inalimwa na kuna miundombinu imara ya kuihudumia na mikoa ya Ruvuma na Rukwa ambako zao hili halijaanza kulimwa. Wajibu wa Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai ni kuona jinsi ya kuwashirikisha wakulima

wadogo katika mipango ya upanuzi wa kilimo cha chai na kufaidika na miundombinu iliyopo na itakayojengwa.

12. Tumepata uzoefu mzuri kwenye mkoa wa Tanga ambako *Usambara Tea Growers Association* na *East Usambara Tea Company* zimewasaidia wakulima wadogo na kuwawezesha kupanua au kuanzisha kilimo cha chai. Napongeza sana jitihada hizi na kuwahimiza mziige na kuzisambaza kwenye maeneo mengine nchini.

13. **Ndugu Mwenyekiti,** Sheria ya Chai ya mwaka wa 1977 iliunda Bodi ya Chai Tanzania na Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai. Kumekuwapo ugumu wa kupata fedha za kugharamia vyombo vyote viwili na baadhi ya Wadau wa Chai wamekuwa wakilalamika kwamba vinawatwisha mzigo usiokuwa wa lazima wakati chombo kimoja kingeweza kuunganisha majukumu yanayofanywa na vyombo hivi viwili. Ningependa kupata maoni na ushauri wenu juu ya suala hili. Maoni na ushauri huo uzingatie maslahi ya wakulima wa chai na manufaa au athari zinazoweza kutokea.

14. Kwa muhtasari, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai mnakabiliwa na changamoto ya:

(a) Kuwalea wakulima wadogo ili waweze kuzalisha chai ya ubora wa hali ya juu na kwa wingi.

(b) Kuongeza uzalishaji wa chai wa wakulima wadogo kutoka kilo 470 kwa hekta za sasa kuelekea kwenye kilo 5,500 kwa hekta unaofanywa na wakulima wakubwa.

(c) Kupanua maeneo yanayolimwa kwa lengo la kuongeza idadi ya wakulima wanaolima chai na wakati huo huo kuongeza kiasi cha chai kinachozalishwa kitaifa.

(d) Kubuni mbinu mbalimbali za kumuwezesha mkulima kujipatia mahitaji yake ya kilimo.

(e) Kikao kijadili hatma ya Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai.

15. **Ndugu Mwenyekiti,** baada ya kusema hayo, ninapenda kuwashukuru tena kwa kunikaribisha kufungua mkutano wenu. Ninawatakia majadiliano yenye manufaa. Sasa natangaza kuwa mkutano huu umefunguliwa rasmi.

Asante sana.